TANGAZO LA SERIKALI NA. 207 La Tarehe 15/3/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA. 287)

# SHERIA NDOGO

(*Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII YA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA ZA MWAKA 2019.

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya za Mwaka, 2019 na zitaanza kutumika rasmi baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo;

"ada ya mtumiaji" maana yake ni ada inayotozwa na Hospitali, Kituo cha Afya au Zahanati, kwa ajili ya huduma za Afya iliyotolewa kwa mtumiaji;

"taasisi' ni pamoja na shule, vyuo, vikundi mbalimbali vilivyosajiliwa kwa mujibu wa sheria au asasi yoyote itakayokuwa imekubaliwa na kuidhinishwa na Bodi;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri iliyoundwa kwa mujibu wa kifungu Na. 88 cha sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za

Wilaya) Sura Na. 287 Toleo la mwaka 2002.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

“huduma za afya” maana yake ni huduma zote za afya zinazotolewa na Hospitali za Serikali au watu binafsi,na zinajumuisha huduma nyingine za afya zilizoanzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za afya ikiwa ni pamoja na vituo vya afya na Zahanati;

“kadi” maana yake ni kadi itakayotolewa na Bodi kwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

“kaya” maana yake ni:-

(a) Mama, baba na watoto au wategemezi wasiozidi wanne wenye umri chini ya miaka kumi na nane; au

(b) Mwanachama yoyote aliyefika umri wa miaka kumi na nane (18) au zaidi na awe na mtoto au bila mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nane (18)

“kituo cha huduma kilichoteuliwa” maana yake ni kituo kinachotoa Huduma za Afya na ni pamoja na kituo chochote kilichoanzishwa au kinachoendesha kwa malengo ya kutoa Huduma za Afya kiwe kinamilikiwa na Halmashauri, Serikali, Asasi ya kidini, mtu au watu binafsi ambacho kinahusika na mfuko wa Afya ya Jamii

“mchango” maana yake ni mchango wa fedha utakaotolewa na mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

“mfuko” maana yake ni mfuko wa Afya ya Jamii.

“Mganga Mkuu wa Wilaya” maana yake ni Daktari ambaye ni Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za huduma za afya katika Halmashauri;

"mwanachama" maana yake ni Kaya ya watu 6, Taasisi ya watu 6 au Asasi ya watu 6, inayochangia kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii;

"malipo ya huduma" maana yake ni malipo yanayotozwa na kituo cha kutolea Huduma za Afya kwa wasio wanachama wa Mfuko.

"tele kwa tele" maana yake ni jazilio la Serikali kwa michango ya wanachama wa Mfuko

Mfuko wa Afya ya Jamii

4. (1) Kutakuwa na Mfuko wa Afya ya Jamii ambao ni mfuko wa hiari wenye lengo la kutoa huduma za afya, ambapo Kaya zitakuwa zikilipia huduma hizo na Serikali itatoa mchango wake wa fedha kama jazilio kwa mchango kutoka kwenye kaya (Tele kwa Tele)

(2) Matumizi ya fedha yatafanywa na kusimamiwa na Bodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Madhumuni na malengo ya Mfuko

5. Madhumuni na malengo ya Mfuko wa Afya ya Jamii yatakuwa kama ifuatavyo:-

(a) kutafuta vyanzo vya fedha kutoka katika jamii kwa ajili ya kutoa huduma bora za afya kwa wanachama;

(b) kutoa huduma bora za afya zinazopatikana kwa kutumia mipango endelevu; na

(c) kuboresha huduma za afya katika jamii kwa kugawanya madaraka na kuzipa nguvu jamii katika kufanya maamuzi na kuchangia katika masuala yanayohusu afya zao.

Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii

6. (1) Kutakuwa na Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya baada ya kupokea mapendekezo kutoka Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri na kuridhiwa na Halmashauri.

(2) Majukumu ya Mratibu wa Mfuko wa Afya ya

Jamii yatakuwa kama ifuatavyo:

(a) kufuatilia, kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya ya Jamii.

(b) kuwa kiungo kati ya Halmashauri, jamii na wadau mbalimbali kwa ushirikiano na mhasibu wa Mfuko, na

(c) kuandaa taarifa za Mfuko wa Afya ya Jamii za robo, na za mwaka pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na Halmashauri.

Muundo wa Bodi

7. (1) Kutakuwa na Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Wawakilishi wanne wa watumiaji huduma za Afya kati yao wawili ni lazima wawe ni wanawake;

(b) Mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za Afya binafsi bila faida,

(c) Mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za afya binafsi kwa faida waliochaguliwa na Halmashauri ya Wilaya kutoka vituo vya kutolea huduma za afya binafsi kwa faida waliochaguliwa miongoni mwao., na

(d) Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji.

(2)

(3) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bodi watachaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa kifungu kidogo (1) a na b hapo juu.

(4) Wajumbe wa kuchaguliwa ndiyo watakao kuwa na uwezo wa kupiga kura na kupitisha maamuzi ya

Bodi.

(5) Wataalam ambao hawatapiga kura ni:-

a) Afisa Mipango wa Halmashauri;
b) Mganga Mkuu wa Halmashauri ambaye atakuwa Katibu wa Bodi ;
c) Mwakilishi mmoja kutoka Hospitali ya Wilaya.
d) Mwakilishi kutoka Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Mkoa.
e) Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii.
f) Mweka Hazina wa Halmashauri

Wajumbe wengine wanaweza kualikwa kama kutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo; lakini hawatakuwa na uwezo wa kupiga kura au kufanya maamuzi.

Sifa za Wajumbe wa Bodi

8 Mjumbe wa Bodi atakuwa na sifa zifuatazo:-

(a) awe raia wa Tanzania mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

(b) awe na umri usiopungua miaka kumi na nane (18) na kuendelea;

(c) awe amehitimu Elimu ya Sekondari kidato cha nne na kuendelea;

(d) awe na uzoefu na amewahi kuonyesha uwezo wake wa kuongoza katika shughuli za huduma ya jamii;

(e) awe na akili timamu;

(f) asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa, na

(g) awe mwanachama hai wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

Kazi za Bodi

9. (1) Ili kufanikisha malengo yake makuu, Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) Bodi ya Afya ya Halmashauri itasimamia masuala na shughuli zote zinazohusu Mfuko wa Afya ya Jamii,

(b) kusimamia Huduma za Mfuko katika Halmashauri,

(c) itafanya kazi kwa kushauriana na Timu ya Uendeshaji ya Huduma za Afya ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa Huduma ya Afya ni bora na ya kitaalamu,

(d) kukusanya na kusimamia mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii,

(e) kupendekeza kwa Halmashauri watu wanaostahili kusamehewa kutoa mchango kwenye Mfuko,

(f) kuweka malengo ya Mfuko,

(g) kupitia taarifa kutoka Kamati za Afya za Kata au chanzo kingine chochote,

(h) kuratibu makusanyo, na kudhibiti mapato na matumizi; na

(i) kupanga mipango ya afya ya mwaka kwa ajili ya kuthibitishwa na Halmashauri;

(2) Bodi katika kutekeleza majukumu yake, itapokea na kutekeleza maagizo ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu

Muda wa Mjumbe kukaa Madarakani

10. (1) Mjumbe wa Bodi atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uzinduzi wa Bodi na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu tu.

(2) Endapo nafasi yeyote ya Mjumbe wa Bodi itaachwa wazi kwa sababu ya kifo, kujiuzulu au kwa sababu nyingine yeyote ile, Mjumbe mwingine atachaguliwa kujaza nafasi hiyo iliyoachwa wazi.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2), haitaruhusiwa kuchagua mjumbe mwingine iwapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita.

Akaunti ya Mfuko

11. (1) Kutakuwepo na akaunti ya Mfuko wa Afya ya Jamii ambapo fedha zote zitakazokusanywa kwa ajili ya Mfuko zitahifadhiwa na kutolewa.

(2) Wawekaji saini wa akaunti ya Mfuko watachaguliwa na Bodi na watakuwa ni: mmoja kutoka kundi "A" na "B" na kwa namna yoyote ile hakuna pesa zitakazotolewa kwenye akaunti ya mfuko bila saini ya mmojawapo kutoka kundi "A" na "B".

(3) Watia saini kwenye hundi za Mfuko watakuwa kama ifuatavyo:-

a. Mwenyekiti wa Bodi na Mjumbe mmoja wa Bodi ambao watakuwa Kundi "A"; na

b. Katibu wa Bodi ambaye atakuwa ni Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya na Mweka Hazina wa Halmashauri ambao watakuwa Kundi "B"

(4) Kila baada ya miezi mitatu, Bodi itakuwa inaandaa na kutoa taarifa ya akaunti ya Mfuko na kuiwasilisha kwa Halmashauri,

(5) Akaunti ya Mfuko itakaguliwa na Wakaguzi waliochaguliwa kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za Serikali.

Matumizi ya

12. Fedha zitakazokusanywa na Mfuko zitatumika kwa

Fedha za Mfuko

madhumuni yafuatavyo:-

(a) masuala yanayohusiana na afya yaliyotajwa katika mpango kabambe wa afya wa Halmashauri na kuidhinishwa na Halmashauri; na

(b) suala au shughuli yoyote muhimu ya afya itakavyoonekana inafaa na kama itaidhinishwa na Bodi.

(c) kulipa mawakala asilimia tano(5%) ya fedha waliyokusanya.

Vyanzo vya Mapato

13. Vyanzo vya mapato ya Mfuko vitatokana na:-

a) fedha zote zitakazopokelewa kutokana na michango ya wanachama,

b) fedha za tele kwa tele,

c) ruzuku kutoka kwenye Halmashauri na Serikali Kuu,

d) wahisani mbalimbali kutoka ndani na nje ya Halmashauri,

e) michango ya watu binafsi wanaoishi ndani na nje ya Halmashauri,

f) malipo ya fedha ya wasiokuwa wanachama wa Mfuko kwa kupata huduma ya afya,

g) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kutokana na makusanyo ya fedha katika vituo vya Afya,

h) fedha zozote halali ambazo Mfuko unaweza kupata kutoka mahali pengine popote.

Mipango na Matumizi

14. (1) Bodi itaandaa mpango na bajeti wa mwaka, miezi miwili kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha wa Halmashauri, kwa kuonyesha

kiwango kinachotarajiwa kupatikana na mgawanyo wa fedha kwa ajili ya utoaji huduma za afya na maendeleo katika maeneo ya Halmashauri.

(2) Bodi inaweza kuandaa bajeti ya nyongeza kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo na kama mazingira yataruhusu;

(3) Mipango ya bajeti ya Mfuko itaandaliwa kulingana na utaratibu kama ilivyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) na (2) hapo juu, ambayo ni lazima iwasilishwe kwa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa.

Usimamizi wa Mfuko

15. Usimamizi na Uendeshaji wa Mfuko utakuwa chini ya:-

(a) Halmashauri ya Wilaya, kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri katika ngazi ya Halmashauri,

(b) Kamati ya Maendeleo ya Kata kupitia Kamati ya Afya ya Kata, katika ngazi ya Kata; na

(c) Serikali ya Kijiji kupitia Kamati ya Huduma za Jamii, katika ngazi ya Kijiji.

(d) Kamati ya usimamizi ya kituo cha afya na zahanati

Taarifa ya Fedha

16. Bodi itatakiwa kuandaa taarifa ya mwaka ya mapato na matumizi ya fedha na kuwasilisha kwa Halmashauri, mwezi mmoja baada ya mwaka wa fedha wa Halmashauri.

Utoaji wa Huduma za Afya.

17 Kila mwanachama:-

a) atakuwa na haki ya kisheria kupata Huduma ya Afya ndani ya eneo la Halmashauri au eneo lingine lolote kwa kadri itakavyo kubaliwa,

b) atakuwa na haki ya kutoa mapendekezo kuhusu Huduma za Afya kupitia Kamati

husika ambayo yatafanyiwa kazi na Bodi; na

c) atashirikishwa kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa Huduma za Afya katika eneo la Halmashauri.

Kiwango cha Mchango au Ada ya Mwanachama kwa kila kaya

18. (1) Mtu yeyote atakayetaka kuwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii atapaswa kulipa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Kila Kaya itachangia kwa mwaka mchango wa shilingi elfu thelathini (30,000/=).

(b)Kwa mtu mmoja pekee mwenye umri wa kuanzia miaka kumi na nane (18) atachangia mchango wa shilingi elfu sita (6,000/=) kwa mwaka

(c) Mwanafunzi wa Sekondari aliyeko bweni atachangia shilingi elfu mbili (2,000/=) kwa mwaka.

(2)Viwango hivi vinaweza kufanyiwa marekebisho na Halmashauri wakati wowote iwapo itaonekana kuna umuhimu wa kufanya marekebisho hayo.

Muda wa uanachama na ukomo wa Uanachama

19. (a) mtu yeyote ataendelea kuwa mwanachama wa mfuko wa afya ya jamii kuanzia tarehe aliyolipa ada yake ya uanachama, na

(b) uanachama wa mtu utafikia mwisho wa Mwaka hadi Mwanachama

(c) atakapotimiza masharti ya kifungu (a) hapo juu.

(d) bila kuathiri masharti ya kifungu (b) mwisho wa mwaka wa mwanachama utahesabika

kuwa ni miezi kumi na mbili tangu tarehe ambayo mwanachama alilipa ada yake ya uanachama

Malipo ya Papo kwa Papo

20. (1) Mtu yeyote ambaye hatakuwa Mwanachama wa Mfuko huu atalipa malipo ya papo kwa papo kila atakapoenda kupata matibabu katika Kituo cha kutolea Huduma za Afya,

(2) Malipo ya Papo kwa Papo yatalipwa kama ifuatavyo;

(a) shilingi elfu tano (5,000) katika Huduma za Afya zinazotolewa na Zahanati katika eneo lolote la Halmashauri.

(b) shilingi elfu saba (7,000) kwa huduma za afya zinazotolewa na kituo cha afya kilichopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya na gharama nyingine zitakuwa kama zilivyo ainishwa katika será ya uchangiaji wa huduma ya Afya

(c) shilingi elfu kumi na mbili (12,000) kwa huduma za afya zinazotolewa na Hospitali ya Wilaya na gharama nyingine zitakuwa kama zilivyoainishwa katika sera ya uchangiaji wa huduma ya Afya

Utaratibu wa Misamaha

21. Misamaha kwa wasioweza kulipia gharama za matibabu utatolewa na kulipwa na Halmashauri baada ya kuzingatia utaratibu ufuatao:-

(a) Serikali ya Kijiji katika vikao vyake itawatambua, kuwajadili na kupeleka kwa Kamati ya Maendeleo ya Kata mapendekezo ya orodha ya majina ya watu wanaostahili kupewa Msamaha,

(b) Kamati ya Maendeleo ya Kata itawajadili wale wasioweza kulipia gharama na

kuthibitisha orodha yao na kuiwasilisha kwa Bodi, na

(c) Bodi ya afya itapokea na kujadili mapendekezo husika na kuyawasilisha pamoja na gharama zake kwa Halmashauri kwa ajili ya kulipiwa.

Utoaji wa Kadi kwa Mwanachama

22. (1) Kila mwanachama wa Mfuko atapewa Kadi baada ya kulipa mchango wake kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 18 cha Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa kuzingatia Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii sura ya 409 kila mtu atakayesamehewa kulipa mchango atapewa kadi ya Uanachama na Halmashauri italipa gharama ya kadi hiyo.

Hati rasmi

23 (1) Halmashauri itatengeneza Hati Rasmi ambayo itapitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri.

(2) Hati hiyo itaanzisha
(i) Bodi ya huduma za Afya za Halmashauri,
(ii) Kamati ya Afya ya Kata,
(iii) Kamati ya Afya ya Kituo cha Afya
(iv) Kamati ya Zahanati

Hati hiyo itaelezea muundo, sifa za wajumbe, majukumu ya bodi na kamati hizo za Afya.

Makosa

24. (1) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote endapo:-

a) atakwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi;

b) atafanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi na Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi.

c) atatumia vibaya mali na rasilimali za Mfuko

d) atashindwa kwa uzembe kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

e) atazuia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Adhabu

25. Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwiili au vyote faini na kifungo kwa pamoja.

Likiri na Mhuri wa Halmashauri ya wilaya ya mbeya umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la kikao cha Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kilichofanyika tarehe …… mwezi….mwaka…..mbele ya:-

STEPHEN E. KATEMBA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya*
*Mbeya*

MWALINGO MWAYONGO KISEMBA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya*
*Mbeya*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
5Machi, 2018

SELEMANI S.JAFO (MB)
*Waziri wa Nchi-or Tamisemi*